**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**WIZARA YA VIWANDA NA BIASHARA**
**BODI YA USIMAMIZI WA STAKABADHI ZA GHALA**

**TANGAZO KWA UMMA**

Bodi ya Usimamizi wa Stakabadhi za Ghala (WRRB) ni Taasisi chini ya Wizara ya Viwanda na Biashara iliyoundwa kwa **Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339.** Bodi pamoja na mambo mengine imepewa jukumu la kutoa leseni ya Uendeshaji wa Ghala.

Bodi inapenda kuzitaarifu Kampuni zenye nia ya kuendesha ghala **kwa msimu wa mwaka 2026/2027 wa mauzo ya zao la korosho** kupitia Mfumo wa Stakabadhi za Ghala kuwasilisha dhamira zao. Kwa kampuni zenye sifa zitawasilisha dhamira zao kupitia kiunganishi https://forms.gle/gfH9zbgvkN1vxFHc6 pamoja na kuambatisha nyaraka zifuatazo;

i. Cheti cha usajili wa kampuni *(Certificate of Incorporation);*
ii. Consolidated form (BRELA);
iii. Hati ya uanzishwaji wa kampuni ( MEMARTS);
iv. TIN na Leseni ya biashara;
*v.* Taarifa ya Mwaka ya Kampuni *(Annual return)*
vi. Tax clarence;
vii. Taarifa ya ukaguzi ya fedha *(audited financial accounts)* ya karibuni ya kipindi cha miaka miwili;
viii. Taarifa ya benki *(bank statement)* ya kipindi cha miezi sita inayoishia tarehe 07 Septemba 2026;
ix. Barua ya dhamira ikiainisha Mkoa na Wilaya anaotarajia kufanya kazi.

Mwisho wa kuwasilisha dhamira ni tarehe **04 Septemba 2026 saa 10:00 jioni.** Kampuni ambayo haitawasilisha dhamira yake ndani ya muda uliopangwa haitaruhusiwa kushiriki kwenye usaili na itakosa sifa ya kuendesha Ghala la zao la korosho kwa msimu wa mwaka 2026/2027.

Usaili utafanyika Mkoani Mtwara kuanzia tarehe **07 Septemba 2026 - 11 Septemba 2026** katika ukumbi wa mikutano wa Bodi ya Korosho Tanzania kulingana na ratiba itakayotolewa kabla ya tarehe ya usaili**.**

Baada ya usaili kukamilika na matokeo kutangazwa, Kampuni zitakazokuwa zimefaulu ndizo zitakazoruhusiwa kuendelea na mchakato wa maombi ya leseni kwa kuzingatia vigezo na masharti kwa mujibu wa Sheria ya Stakabadhi za Ghala Sura 339.

Kwa maelezo zaidi tafadhali wasiliana na Bw. Nasri Khea kwa simu namba 0712950117 barua pepe nasri.khea@wrrb.go.tz na Emmanuel Mlenge kwa simu namba 0683177007 barua pepe emmanuel.mlenge@wrrb.go.tz.

Imetolewa na;
**MKURUGENZI MTENDAJI**
**Agosti 24, 2026**